

MAIR

**Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji
MKUKUTA - 2006/2007**



**Nguzo ya Kwanza:
Kukuza Uchumi na
Kupunguza Umaskini wa Kipato**

Nguzo ya Kwanza ya MKUKUTA inahusu shughuli za “Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato”. Matokeo ya jumla ni “kukua kwa uchumi ambao ni endelevu, unaofikia watu wengi na kwa uwiano unaokubalika”

Malengo

- Kuhakikisha kunakuwapo usimamizi mzuri wa uchumi
- Kuchochea ukuaji wenye msingi mpana na endelevu
- Kuimarisha usalama wa chakula
- Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanaume na wanawake vijijini
- Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanaume na wanawake mjini
- Kutoa nishati ya kuaminika na rahisi kwa watumiaji.

Changamoto kuu

Ili kufikia malengo, inatupasa kuzishughulikia changamoto zifuatazo:

- Ukuaji wa kasi zaidi wa uchumi
- Mahusiano bora zaidi ya uchumi mkubwa na ule wa ngazi za chini ili ukuaji uweze kuwanufaisha zaidi watu maskini.
- Sera zinazooana vizuri zaidi
- Jinsi ya kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma za aina tofautinje ya nchi
- Upatikanaji nishati ya uhakika
- Maendeleo bora zaidi ya vijijini na kilimo
- Mipangilio mizuri zaidi ya soko la ajira
- Matumizi bora na endelevu zaidi ya maliasili

Mambo Tuliyojifunza na Hatua za Kuchukua

Hatua zinazopaswa kuchukuliwa zinahusisha kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu. Maeneo muhimu yafuatayo yanahitaji hatua za makusudi:

Kilimo

Sera ya kilimo haina budi kuwa na malengo ya aina mbili. Moja likihusisha kuinua uzalishaji mdogo wa kilimo kama sehemu ya mkakati wa kupunguza umaskini. Na lengo la pili ni kukuza uzalishaji mkubwa wa sekta ya kilimo cha kibiashara iliyopatiwa msukumo na nguvu mpya. Njia nyingine za kuinua uzalishaji wa sekta ya kilimo ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa taarifa za masoko ya bidhaa za kilimo na kuongeza kasi ya mwitikio wa sekta binafsi katika kuzitumia taarifa hizo.

Shughuli za Kijijini zisizo za Shamba:

Shughuli za vijijini zisizo za mashambani hususan kwenye usindikaji na utoaji huduma, hazina budi kukuzwa kwani ni fursa muhimu katika kuongeza ajira. Mkakati wa aina hii huweza kufanikiwa katika maeneo yenye barabara nzuri, umeme na mawasiliano ya kuaminika.

Kiwango cha elimu na miundombinu ya msingi ndivyo vichocheo muhimu katika kukuza shughuli za kiuchumi zisizo za mashambani kwenye maeneo ya vijijini. Serikali imedhamiria kuboresha maeneo haya.

Huduma za Fedha

Serikali itaongeza kasi ya utekelezaji wa awamu ya pili ya Maboresho ya Sekta ya Fedha. Sekta hii itaendelea kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kutoa huduma za kutosha na ambazo watu wengi wanaweza kuzimudu.

Nishati

Kuna umuhimu wa kuwa na vyanzo mbadala vya nishati. Hili linaweza kufanikishwa kwa kukuza ushirikiano wa kikanda katika sekta ya nishati, na kwa kutekeleza kwa Mpango Mkuu wa Sekta ya Nishati.

Ajira

Kuna uhitaji mkubwa wa kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Vijana, Sera ya Ajira ya Taifa, na Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii. Utekelezaji wa sera hizi utasaidia kuongeza fursa za ajira sambamba na kuandaa mazingira bora zaidi kwa ajili ya ajira binafsi.

Fedha za umma

Hapana budi kuwapo msisitizo (a) katika kufikia na kudumisha kiwango cha kuridhisha cha usimamizi bora wa fedha na uwajibikaji na (b) kuboresha ukusanyaji, upangiliaji na utumiaji wa raslimali.

Katika ngazi ya kimataifa, kuna umuhimu wa kuhimiza diplomasia ya kiuchumi yenye kulenga (a) kuvutia masoko na wawekezaji wa nje ya nchi (b) kujadiliana na wahisahi juu ya mikopo yenye riba nafuu pamoja na kushawishi kufutiwa madeni.

Maliasili na Mazingira:

Juhudi zinahitajika ili:

- Kuboresha usimamizi katika sekta
- Kuongeza jitihada za upandaji miti
- Kutekeleza malengo ya ukusanyaji wa maduhuli
- Kuimarisha Kitengo cha Usimamizi wa Misititu
- Kuzuia uvunaji haramu

Msaada zaidi unahitaji katika kuwezesha ukusanyaji na uchanganuzi wa taarifa kwa kuzingatia uendeleu wa mchango wa maliasili kwa maendeleo ya Taifa

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Wizara ya Fedha na Uchumi,

S..L.P. 9111, Dar Es Salaam

Simu: +255 2111174, Fax: 21103226

Barua Pepe: mkukuta@gmail.com; Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz